**HOTUBA YA HAKIMU MKAZI MFAWIDHI OSMUND N. NGATUNGA**

**SIKU YA SHERIA NCHINI (LAW DAY), CHUNYA**

**TAREHE 01 FEBRUARI, 2018**

*Mhe. Rehema Madusa Mkuu wa Wilaya,*

*Wahe. Mahakimu wenzangu toka ngazi zote,*

*Mhe. Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya,*

*Mhe. Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri,*

*Wahe. Wakuu wa vyombo vya ulinzi na Usalama,*

*Ndg. Upendo B. Mahenge, Afisa Tawala wa Mahakama,*

*Wahe. Viongozi wa Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma,*

*Wahe. Madiwani,*

*Wahe. Wakili wa Kujitegemea na Wanasheria wa Halmashauri,*

*Wahe. Waendesha Mashtaka,*

*Wahe.Viongozi wa Dini kutoka Madhehebu mbalimbali,*

*Wahe. Viongozi wa Vyama vya Siasa,*

*Watumishi wa Mahakama ngazi zote,*

*Wahe. Wageni waalikwa wote mliopo,*

*Mabibi na Mabwana*

## 1.0 Utangulizi

Awali ya yote, naomba wote tusimame kwa dakika moja kumkumbuka Mhe. Eliah Akimu Mwamelo, Hakimu Mkazi Mahakama ya Mwanzo Makongolosi na watumishi wengine wa Chunya waliotangulia mbele ya haki tangu tukutane hapa mwaka 2017. Asanteni. Napenda sasa kuwatakia heri ya mwaka mpya na kuwakaribisha nyote katika adhimisho la siku hii.

## 2.0 Tehama na umuhimu wake

Mhe. Mgeni Rasmi na Wageni Waalikwa,

Kauli mbiu ya adhimisho mwaka huu ni:- **"Matumizi ya TEHAMA katika utoaji haki kwa wakati na kwa kuzingatia Maadili"**

Kwa maneno mengine kauli mbiu ina lengo la kutuonyesha matumizi ya **TEHAMA** katika utoaji huduma za jamii, hasa utoaji haki na kuimarisha uwazi na maadili.

TEHAMA ni nini? Ni Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Kihistoria, dhana hii imegawanyika katika makundi mawili ambayo ni **analogia** na **digitali**.

Analogia ni upashanaji habari isiyotumia vifaa vya kielekitroniki kama typewriter, posta, mkono kwa mkono, matumizi ya karatasi, mafaili ya kawaida n. k.

Digitali ni upashanaji wa habari kwa kutumia vifaa vya mawasiliano, na mifumo mtandao au program, (kielekitroniki) ili kugawana habari kupitia tovuti (*www.judiciary.go.tz*), barua pepe (*info@judiciary.go.tz*), faksi, video confencing, simu (smart phones), scanner, mitandao ya kijamii kama facebook, whatsapp, twiter, instagram, blogs, you tube n.k.

Awali na pahala pengine Mahakama za Mwanzo nyingi hutumia mfumo wa analogia katika kuwasiliana au kupashana habari. Kwa mfano hutumia barua, usajili wa mashauri, namna ya usikilizaji wa mashauri, uandaaji wa nyaraka kwa ajili ya malipo, kusambaza hati za wito Mahakamani n. k.

Ispokuwa kwa ngazi ya Mahakama za Wilaya, Mahakama Kuu, na Mahakama ya Rufaa kwa kiasi kikubwa hutumia mfumo wa Mahakama mtandao (*e-judiciary*) katika kusajili mashauri, kutoa hati za kuitwa shaurini kama njia ya mawasiliano ili kufanikisha shughuli zake za kila siku.

Mahakama Maboresho kupitia Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Mkataba wa Huduma kwa Mteja 2002 na Mpango Mkakati wa Mahakama 2015-2020 inakusudia pamoja na mambo mengine kutumia TEHAMA katika kuboresha misingi ya utawala bora, amani na utulivu, uthabiti na umoja wa kitaifa ili kuchochea maendeleo ili kufikia lengo lake la kuwa na Mahakama iliyokaribu na inayofikiwa na wananchi katika kutoa huduma za utoaji haki Nchini.

**3.0 Jukumu la utoaji haki**

Kama vilivyo vyombo vingine vya dola ambavyo vimekasimiwa mamlaka ya Kikatiba ya **utendaji (Utawala), uwakilishi, kutunga sheria na kuisimamia Serikali (Bunge)** Mahakama imepewa jukumu la Kikatiba na kisheria la **utoaji haki**. Ina **mamlaka yenye "kauli ya mwisho" ya utoaji haki** kwa wananchi kwa mujibu wa **Ibara ya 4, 107A, 107B** ya Katiba yetu.

Kwa mujibu wa Ibara ya 107B ya Katiba ya Nchi, Mahakama inapaswa ilinde uhuru, haki, hadhi na mamlaka ya Kikatiba dhidi ya mihimili mingine ya dola na wananchi. Dhana ya uhuru wa Mahakama imejikita hasa katika mambo ya ki-utawala, fedha na utendaji wake hasa wakati shauri linaposikilizwa na kuamuliwa bila kuathili ibara ya 8 na 146 ya Katiba ya Nchi.

TEHAMA ina lengo, pamoja na mambo mengine, kuharakisha upatikanaji wa huduma mbalimbali zitolewazo na Mahakama ili kukidhi Dira yake isemayo **"Haki sawa kwa wote na kwa wakati".** Mbali na kutumia TEHAMA pia tumekusudia kutumia Mahakama itakayotembea yaani kuna gari maalum litakalotumika kufika sehemu mbalimbali ndani ya Wilaya yetu ili kwenda kusikiliza mashauri na kutoa elimu. Mahakimu, watunza kumbukumbu na Katibu Muhtasi watakao tekeleza jukumu hili katika eneo letu wameshateuliwa.

TEHAMA itafanikisha kurekodi ushahidi, umalizikaji mashauri haraka, mazingira mazuri ya utendaji kazi, kupata huduma za mahakama bila urasimu, kupata nakala za mwenendo na uamuzi wa Mahakama kwa wakati.

Ni imani ya Mahakama kwamba endapo TEHAMA itatumika kama ilivyokusudiwa itasaidia kuondoa misemo ya wanazuoni isemayo "**haki siyo tu itendeke bali ionekane imetendeka"**, pia **"haki iliyocheleweshwa ni haki iliyonyimwa"** lakini vilevile **"haki iliyoburuzwa ni haki iliyozikwa"**.

## 4.0 Faida ya matumizi ya TEHAMA kama njia ya kuimarisha ubora wa utaji haki

Kama nilivyoeleza hapo awali, endapo TEHAMA itatumika kwa usahihi wake katika sheria itasaidia uboreshaji wa kazi za utoaji haki mahakamani.

a. Hupunguza gharama kwa kiasi kikubwa. Wananchi watakuwa na uwezo wa kufungua mashauri mbalimbali na kufuatilia mwenendo wake wakiwa nyumbani.

b. Huwezesha kutatua au kusikiliza shauri kwa muda mfupi na kwa gharama nafuu.
c. Huwezesha utoaji nakala za hukumu, mwendendo wa shauri kirahisi na kwa uhakika na pia huwezesha mashauri kusikilizwa kwa kutumia video conference. Shahidi halazimishwi kufika mahakamani hasa wale walio mbali au nje ya Nchi.
d. Changamoto ya uhaba wa Mahakimu hupungua. Kwa kutumia TEHAMA kuna uwezekano mkubwa wa hakimu wa eneo moja akiwajibika katika Mahakama nyingine kadhaa za maeneo ya jirani.
e. Hupunguza mianya ya rushwa, urasimu na usumbufu kwa wananchi. Kwa mfano baadhi ya watumishi huchelewesha mashauri kwa maelezo kuwa faili husika halionekani. TEHAMA huondoa majibu ya aina hiyo kwa sababu taarifa muhimu za mashauri huifadhiwa katika mfumo salama wa kompyuta.
f. Husaidia usalama, usahihi wa kumbukumbu, kutunza siri za ofisi, pia husaidia mawasiliano ya watu wengi kwa wakati mmoja.
g. Inarejesha imani kwa wananchi na wadau wa Mahakama.
h. Hupunguza matumizi ya karatasi, kalamu, na majalada ya kawaida.
i. Hupunguza malalamiko kwa wadaawa, washtakiwa na walalamikaji kuhusiana na maamuzi ya Mahakama hasa kwenye mfumo wa kuandika mwenendo wa shauri.

## 5.0 Changamoto

1. Ukosefu wa miundombinu ya Mahakama hasa ngazi ya Mahakama za Mwanzo.
2. Ukosefu wa watumishi wanaoweza kutumia TEHAMA katika shughuli za Mahakama.
3. Mahakama zilizo nyingi zipo vijijini na kwa kiasi kikubwa mtandao wa umeme haujafika.
4. Mfumo wa usajili wa mashauri kuwa na uwezo mdogo (main server) husababisha kuzidiwa.

## 6.0 Mikakati na mipango ya baadae ya Mahakama

Kuna umuhimu wa kuongezwa kwa rasilimali fedha, wataalam na kutoa mafunzo endelevu kwa watumishi waliopo ili kuimarisha matumizi ya Tehama na mwishowe kuondokana kabisa changamoto zilizopo.

Kuhakikisha kuwa taarifa zote muhimu za mashauri zinapatikana kwenye mfumo mzima wa usimamizi wa mashauri (Full Case Management System).

Kuboresha miundombinu ya Mahakama itakayoweka mfumo Mahakama mtandao (*e-judiciary*) ili taarifa zote muhimu zipatikane kwenye tovuti ya Mahakama.

Kuweka umeme kwenye majengo yasiyo na nishati ya umeme kwa kutumia mradi wa umeme vijijini (REA).

Kuboresha mfumo wa ukusanyaji wa maduhuri au Government Electronic Gateway (GEPG).

Kutumia Mahakama inayotembea ili kusikiliza na kuamua mashauri kwa haraka na kwa wakati.

Tunakusudia kutumia video conference wakati wa kusikiliza mashauri ili kupunguza usumbufu kwa watuhumiwa na mashahidi kufika Mahakamani.

**7.0 Hitimisho**

Lengo tulilojiwekea mahakama ni kusikiliza na kutoa maamuzi mashauri mbalimbali yanayofunguliwa katika Mahakama zetu kwa wakati na katika mazingira ya haki, usawa, weledi, uwazi na yanayozingatia maadili ya utendaji kazi.

Hivyo basi, endapo TEHAMA itatumika kwa usahihi itaongeza ufanisi, tija, itaboresha utoaji huduma na kuharakisha kufanya maamuzi, hupunguza gharama, hupunguza vitendo vya rushwa, hutunza siri za ofisi na kumbukumbu.

Waheshimiwa Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana, nawashukuru sana kwa kunisikiliza.

Asanteni.

**O. N. Ngatunga**

**HAKIMU MKAZI MFAWIDHI**

**CHUNYA**